

MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21 – 31 MEI, 2019 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 01- 10 JUNI, 2019.

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 21 – 31 MEI, 2019.

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilidhoofika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika. Hali hii ilisababisha ukanda wa mvua (ITCZ) kupanda kuelekea kaskazini mwa dunia na kuwepo katika nchi yetu hususan maeneo ya ziwa Viktoria. Joto la bahari la juu ya wastani katika eneo la kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi liliendelea na kupelekea upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka Kusini Mashariki hususani pwani ya kaskazini mwa Tanzania. Joto la bahari la chini kidogo ya wastani liliendelea katika eneo la Kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii ya mifumo ilipelekea kuimarika kwa mifumo ya mvua kwa baadhi ya maeneo ya nchi yetu hususani katika ukanda wa ziwa Viktoria.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21 –31 MEI, 2019

Mwenendo wa viashiria vya hali ya hewa hapo juu, vilipelekea vipindi vya mvua kubwa zilizoambatana na ngurumo za radi katika maeneo ya ukanda wa ziwa Viktoria hususani magharibi na mashariki mwa Ziwa Victoria pamoja na ukanda wa pwani ya kaskazini mwa Tanzania. Aidha, maeneo ya nyanda za juu Kaskazini Mashariki, vipindi vichache vya mvua zilizoambatana na ngurumo vilijitokeza.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 01 - 10 JUNI, 2019.

2.1 VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 01 - 10 JUNI, 2019.

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarika. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda wa mvua (ITCZ) kupanda kuelekea kaskazini mwa dunia na kuwepo katika nchi yetu hususani maeneo ya ziwa Viktoria. Joto la bahari la juu ya wastani la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuendelea, hali hii inatarajiwa kusababisha kufanyika kwa migandamizo midogo ya hewa pamoja upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka kusini mashariki na kuelekea pwani ya kaskazini mwa Tanzania, hivyo kusababisha mvua kubwa hususani katika visiwa vya Unguja na Pemba. Joto la bahari la chini kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la Kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii ya mifumo inaweza kupelekea kuimarika kwa mifumo ya mvua kwa baadhi ya maeneo ya nchi yetu hususani katika ukanda wa ziwa Viktoria na magharibi mwa nchi.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE (01 - 10 JUNI, 2019.)

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara): Mvua zinazoambatana na ngurumo katika baadhi ya maeneo hususani siku tano za mwanzo wa dekad zinatarajiwa.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro): Mvua katika maeneo machache hususani katika siku tano za mwanzo wa dekad zinatarajiwa.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Mvua katika maeneo machache, nakuongezeka kwa mvua siku mbili za mwisho wa dekad hususani katika visiwa vya Unguja na Pemba zinatarajiwa.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache katika mkoa wa Kigoma zinatarajiwa na katika mikoa ya Tabora na Katavi hali ya ukavu kwa ujumla.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Makavu kwa ujumla.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa): Makavu kwa ujumla.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Makavu kwa ujumla

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Makavu kwa ujumla

Imetolewa na; **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**